THE GUARDIAN · Page 1.

# Govt seeking IFAD fishing ships grant

By Henry Mwangonde

CCM presidential candidate Dr John Magufuli yesterday promised to purchase eight fishing ships if re-elected, aimed at modernizing the industry, equip fishermen with technology to harvest more and improve their lives.

Addressing a rally at Mwanakalenge grounds in Bagamoyo, Coast region, he said that talks had reached a good stage with the International Fund for Agricultural Development (IFAD) to obtain a grant for the purpose, noting also that four of the ships will be stationed in Zanzibar.

"We are determined to improve the lives of fishermen, that is why we have put in place various initiatives aimed at facilitating this because we have their welfare at heart," he declared.

The government similarly plans to revive the Tanzania Fisheries Corporation (TAFICO), detailed to set up fish processing industries in Bagamoyo and elsewhere, he said.

Dr Magufuli said the government has already repossessed properties worth 118bn/- which belonged to TAFICO and were grabbed by corrupt individuals.

Back in May, the government enacted the Deep Sea (Fisheries Management and Development) Act, 2020 envisaging the setting up of the Deep Sea Fishing Authority.

The law was aimed at sorting out challenges in the fishing sector, including illegal, unreported

TURN TO PAGE 2

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 3.

# * Afrika Mashariki yaoneshwa fursa sekta ya ngozi, matunda

Na Theopista Nsanzugwanko

RIPOTI ya Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) imebainisha fursa zilizopo katika bidhaa za ngozi na mboga katika jumuiya hiyo na kuonesha nchi hizo zinapoteza mabilioni ya fedha kutoka na kuzorota kwa sekta hiyo.

Ripoti hiyo iliyotolewa kwa ushirikiano na Taasisi ya GIZ ya ujenzi wa mnyororo wa thamani katika bidhaa zitokanazo na ngozi, matunda na mboga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki' ilizinduliwa Oktoba 8, mwaka huu.

Msimamizi wa Mradi EABC, Sylvester Kimeu, alisema ukanda huo una utajiri mkubwa wa rasilimali za bidhaa za ngozi ukiwa na mifugo aina ya ngombe, kondoo na mbuzi zaidi ya milioni 188.1.

Alisema licha ya mahitaji ya sasa ya ukanda huo kwa kila mwezi jozi 600,000 za viatu vya kiwandani, lakini uzalishaji ni jozi za viatu 60,000 tu kwa mwezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa EABC, Dk Peter Mathuki alisema sekta ya ngozi imeendelea kushuka kwa muda mrefu kutokana na uwapo mkubwa wa viatu vya mitumba kutoka nje ya ukanda huo.

"Uagizaji wa viatu vya mitumba una gharama za chini kuliko gharama za uzalishaji kwa wazalishaji wa ndani na hivyo kupunguza soko katika sekta hiyo ambayo bado haijapata fedha za kutosha," alisema Mathuki.

Ripoti hiyo inaonesha kuna fursa kubwa ya kuongeza ukuaji wa uchumi kupitia kilimo cha bustani, kwani usafirishaji wa bidhaa za mboga na matunda bado ni kwa kiasi kidogo.

"Kama ilivyoelezwa, wakulima wengi wana fedha chache kwa ajili ya kununua pembejeo huku ukosefu wa vifaa vya usindikaji karibu na vyanzo vya mazao yao pia umezuia EAC kunufaika kikamilifu na sekta hiyo.

"Miundombinu inayofaa kwa uuzaji na uhifadhi baada ya kuvuna unaweza kupunguza hasara ambazo wakulima wa bustani wanakabiliwa nazo," alisema Mathuki.

Ripoti hiyo inapendekeza serikali za nchi wanachama wa EAC kusitisha ushuru wa kuagiza na ushuru wa ongezeko la thamani kwenye mbegu na miche inayoingizwa kutoka nje pamoja na pembejeo nyingine.

# * Uga
# za J

Na Theopist
Nsanzugwa

UAMU
Magu
vituo
kufanya bias
umeivutia U
nayo imeam
vituo hivyo r
Wizara ya
Maendeleo ya
humo, ipo kati
kuanzisha vitu
maeneo mbalir
godi ya madini
Kaimu Mku
ti wa Jiolojia na
nchini Uganda,
juzi alisema wa
vituo vya ma
limechukuliwa
ambayo imenu
kikubwa na uta
"Tanzania i
katika sekta nd
barani Afrika,
hivi karibuni t
vituo vya unur
kuongeza kuw
daa andiko la
wizarani amba
mbele ya Baraz
idhinishwe.



Mwonekano wa ha
mita 11.85 baada
baina ya mikoa ya
mara ambayo mad
Wetu).

## Waliodah

Na Lucy Lyatuu

TUME ya Vyu
Tanzania (TC
sema awamu
udahili kwa ngazi
ya kwanza katika
elimu ya juu kwa
masomo 2020/202
wa Oktoba 18 mw
Taarifa ya TCU il
jana, ilieleza kuwa k
endelea ni vyuo kuc
kuidhinisha maombi
yaliyopokelewa vyuo
Katibu Mtendaji
fesa Charles Kihamp
alieleza kwenye taar

UHURU UK 19.

# Wafugaji wataka askari TANAPA waache kuwachapa viboko, kuwatoza faini

**Na MWANDISHI WETU,** *Mkinga*

CHAMA Cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kimelitaka Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), kuacha mara moja kuwabughudhi wananchi wa Kijiji cha Mkota, kilichopo Wilaya ya Mkinga, mkoani Tanga, kwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi haipo kwenye wilaya hiyo.

Januari 15, mwaka huu, Rais Dk. John Magufuli, aliagiza kusitishwa mara moja kwa zoezi la kuvindoa vijiji na vitongoji vinavyodaiwa kuwepo kwenye maeneo ya hifadhi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa CCWT, Jeremia Wambura, baada ya kuwatembelea wafugaji hao na kumweleza adha kubwa wanayoipata kutoka kwa askari wa TANAPA, ikiwemo kuwachapa viboko wanapokwenda kuchota maji na kutoza faini mifugo kinyume na utaratibu.

"Mpeleekeni salamu zangu Kamishina wa Uhifadhi wa TANAPA kwamba, aheshimu tamko la Rais Magufuli, alilolitoa Januari 15, mwaka huu, kwamba wananchi wote wanoishi jirani na hifadhi za taifa na mapori tengefu, wasibughudhiwe na mtu yeyote. Kwa kuwa Rais hajatoa tamko lingine, hakuna mtu yeyote mwenye mamlaka ya kubughudhi wananchi,"alisema Wambura.

Alisema wafugaji hao wamemjulisha kuwa, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, alifanya ziara katika kijiji hicho na kuagiza uongozi wa TANAPA, utumie busara ya kuwaacha wafugaji hao waendelee kutumia maji hayo ya mabwawa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo ili isife kwa kukosa maji, lakini bado hawatekelezi maagizo hayo.

"Nikiwa kiongozi wa wafugaji, siwezi kukubali kuona wafugaji wanabughudhiwa, hasa wale wanaokaa kwenye maeneo ya vijiji, kwa tamko la Rais Magufuli la Januri 15, mwaka huu. Hivyo ninakuagiza Mwanasheria Mkuu wa CCWT, umwandikie kamishina huyo wa TANAPA, barua ya kumtaka aheshimu tamko la Rais hadi hapo atakapotoa tamko jingine," alisema Wambura.

Alisema ametembelea kwenye vijiji vya wafugaji vinavyozuguka hifadhi hiyo katika Mkoa wa Kilimanjaro, hasa wilaya za Same na Mwanga na baadaye Mkinga, iliyopo mkoani Tanga na kwamba, hajaona mnyama yeyote, hata sungura katika maeneo hayo ya vijiji vya wafugaji, ambavyo vinapata adha kubwa ya mifugo yao kukamatwa na kutozwa sh. 100,000 kwa kila mfugo.

Wambura, alitumia fursa hiyo kuwaomba wafugaji hao kuendelea kuwa na imani na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho Ilani yake inatekelezwa na Oktoba 28, mwaka huu, wawapigie kura wagombea wa CCM, ili kero zao aziwasilishe kwenye serikali ya viongozi sikivu na makini.

Wakizungumza na Uhuru, baadhi ya wananchi hao, ambao ni wafugaji, walisema kabla ya mpaka wa hifadhi hiyo kuhakikiwa, eneo la mabwawa ya asili lilikuwa sehemu ya eneo la kijiji, lakini mipaka hiyo mipya imeingiza mabwawa hayo ndani ya eneo la hifadhi, hali inayowapa adha kubwa kupata maji ya matumizi ya nyumbani na mifugo.

Agnes Mollel, alisema wanawake na watoto wanaokwenda kuchota maji kwenye mabwawa hayo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, wanakamatwa na kuchapwa viboko na askari wa hifadhi hiyo, hali inayowasababishia usumbufu mkubwa .

Kwa upande wake, Teu Matagi, alisema anamuomba Rais Magufuli kuwasaidia ili waondokane na adha ya mifugo yao kukamatwa na kutozwa sh. 100,000, kwa mfugo mmoja, hali ambayo imewasababishia umasikini mkubwa, ikiwa ni pamoja na mchungaji kukamatwa na kupelekwa makao makuu ya hifadhi hiyo, yaliyopo Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, bila uwepo wa taarifa yeyote kwa viongozi wa wilaya ya Mkinga wala familia.

Akijibu malalamiko ya wananchi hao, Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano TANAPA, Paschal Shelutete, alikiri kuwepo kwa malalamiko ya wananchi hao na kwamba, mgogoro wao unafanyiwa kazi na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na uongozi wa serikali ya mkoa wa Tanga.



Scanned with CamScanner

KILIMO

# Magu yavuna mafanikio kwenye kilimo, uvuvi na utalii

Na NASHON KENNEDY



Mkurugenzi Mtendaji, Lutengano George Mwalibwa

KUNA msemo kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Wakati kauli hiyo ikielezwa hivyo, wapo wanaodhani kuwa kuwekeza kwenye kilimo ni kujitakia balaa na kwamba hakuna uhakika wa kuvuna kile wanachotarajia.

Lakini kwa Halmashauri ya Magu mkoani Simiyu, hali ni tofauti kutokana na kupata mafanikio makubwa kwenye sekta hiyo na hivyo kuwa miongoni mwa halmashauri iliyowekeza kwenye kilimo chenye tija.

Kama anavyoeleza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya hiyo, Lutengano George Mwalibwa katika mahojiano na gazeti hili hivi karibuni wilayani humo.

Swali: Nini siri ya mafanikio yenu katika sekta ya kilimo?

Jibu: Mafanikio yetu kwenye sekta ya kilimo katika halmashauri yetu yametokana na halmashauri kutekeleza vyema maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kukifanya kilimo kuwa cha kisasa zaidi, cha kibiashara na chenye tija kwa wananchi.

Zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wa Magu wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula kama shughuli yao kuu ya kiuchumi, ambayo kijiografia, wilaya yetu ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,671, ambapo kati ya hizo, kilomita za mraba 1,551 ni maji na kilomita 1,120 ni nchi kavu ambazo zinafaa kwa shughuli za kilimo. Ardhi yetu ina rutuba na hali ya hewa ni nzuri yenye mvua za kutosha kustawisha mazao ya chakula na biashara ya aina mbalimbali.

Swali: Vipi kuhusu upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima? Hali ikoje?

Jibu: Ili kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za zana za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa, hususan katika kuboresha mifumo ya utoaji wa ruzuku na pembejeo, tumewaunganisha wakulima wetu na Benki ya Kilimo na taasisi nyingine za fedha, na upatikanaji wa pembejeo kwa sasa umeongezeka maradufu.

Matumizi ya mbolea kwa wakulima yameongezeka kutoka tani 50,000 mwaka 2015 hadi kufikia tani 156,104 kwa mwaka huu, mbolea za viwanda kutoka tani 20,000(2015) hadi tani 32,242(2020).Kwa upande wa mbegu za mazao ya chakula, upatikanaji wa mbegu hizo umeongezeka kutoka tani 1000 (2015) hadi kufikia tani 1,521,881 kwa mwaka huu na mbegu za mazao ya biashara nazo zimeongezeka kutoka tani 25,025 mwaka 2015 hadi kufikia tani 30,446 kwa mwaka huu.

Kwa upande wa viuatilifu, vimeongezeka kutoka lita 45,000 mwaka 2015 hadi kufikia lita 30,446 kwa mwaka huu na zana za kilimo, majembe ya kukokotwa na ng'ombe yameongezeka kutoka 11,426(2015) hadi kufikia 12,797na pia idadi ya wakulima waliounganishwa na Benki ya Kilimo imeongezeka hadi kufikia wakulima 120 katika kipindi hicho. Aidha idadi ya wakulima waliopata mafunzo imeongezeka kutoka wakulima 320 kwa mwaka 2015 hadi kufikia wakulima 1,599 kwa mwaka huu, haya ni mafanikio makubwa tuliyopata katika sekta ya kilimo katika halmashauri yetu.

Swali:Hali ikoje kwa upande wa sekta za uvuvi na kilimo?

Jibu: Kwa upande wa sekta za mifugo na uvuvi, sekta hizo zimeimarishwa vyema, lengo likiwa ni kuongeza kipato kwa wafugaji na wavuvi ili nao waweeze kutoa mchango wao kwenye pato la mkoa. Mfano katika kipindi cha miaka kitano iliyopta, tumeboresha miundombinu ya mifugo ambapo malambo 15 yamejengwa, majosho ya kuogeshea mifugo 21 yamejengwa, tumeongeza minada ya mifugo kutoka mnada mmoja hadi minne, shamba darasa moja hadi 8 sanjari na kujenga vituo viwili vya uhamilishaji mifugo na pia tumeongeza maafisa ugani ngazi za kata na vijiji kutoka 36 mwaka 2015 hadi kufikia 42 kwa mwaka huu.

Swali: Hali ya udhibiti wa uvuvi haramu ikoje katika halmashauri yako?

Jibu: Tumesimama kidete katika kudhibiti uvuvi haramu ili uvuvi wa kuvua kisheria uwe endelevu, ambapo doria za udhibiti zinazofanywa na vikosi vya udhibiti zimeongezeka kutoka doria 48 mwaka 2015 hadi kufikia doria 192 hadi mwezi Juni mwaka huu.

Idadi ya zana haramu zilizokamatwa zimeongezeka kutoka 381(2015) hadi kufikia zana 4,700 mwaka huu zikiwa na thamani ya Sh 554.7 na watuhumiwa wa uvuvi haramu nao wameongezeka kutoka 14 mwaka 2015 hadi kufikia 80 kwa mwaka huu na tunaendelea kuwadhibiti kwa kutumia vikosi vya doria.

Aidha idadi ya nyavu za kokoro zilipungua kutoka 350 hadi kufikia 250 ka mwaka huu na timba zikiongezeka kutoka timba 250 hadi 750. Changamoto tunayokabiliana nayo katika udhibiti wa uvuvi haramu ni gharama kubwa za uendeshaji wa doria, ukosefu wa vitendea kazi boti ukosefu wa mafuta na ulinzi na kukosa ushirikiano baina ya wananchi na watendaji wachache wa Serikali," anaeleza.

Swali: Vipi kuhusu mali asili na utalii, hali ikoje katika wilaya yako?

Jibu: Kama halmashauri, tumeendelea na mikakati kadhaa iliyoelekezwa kwenye ilani lengo likiwa ni kukuza utalii na kuendeleza mali asili zilizoko wilayani Magu. Nikiri kuwa utalii ni miongoni mwa sekta muhimu zinazochangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla, ambayo pia imetumika katika kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Mikakati tunayoendelea nayo ni pamoja na kuwahamasisha wananchi wetu kutembelea vivutio vya utalii wa ndani kwa kuweka mazingira yatakayowawezesha wawekezaji wa ndani kuendeleza biashara hiyo ya utalii.

Tumewapatia wananchi elimu iliyowafanya kuwa na mwamko mkubwa wa *kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyo kwenye halmashauri yetu. Kwa mfano,* Makumbusho ya Wasukuma ya Bujora, idadi ya watu waliotembelea makumbusho hayo imeongezeka kutoka 5,446 mwaka 2015 hadi kufikia 32,500 kwa mwaka huu na Makumbusho ya kihistoria ya Kageye idadi hiyo imeongezeka katika kipindi hicho kutoka 2,158 hadi 15,670.

Tumeongeza pia eneo la kupanda miti kutoka hekta 508.2(2015) hadi kufikia hekta 3,347 kwa mwaka huu, sanjari na kuongezeka kwa idadi ya miti iliyopandwa kutoka miti 254,107(2015) hadi kufikia jumla ya miti 1,673, 748 (2020) na kuifanya Wilaya ya Magu kuwa ya kijani.

Swali: Una wito ganji kwa wananchi na wadau wa maendeleo kwa ujumla?

Jibu: Nitoe rai kwa wananchi waendelee kuvitembelea vivutio mbalimbali vya utalii tulivyo navyo katika halmashauri yetu, lakini pia wawe mabalozi wazuri kwa wageni wa ndani na wale wa kutoka nje ya halmashauri yetu katika kuvitangaza vivutio mbalimbali vya utalii tulivyo navyo na kuiwezesha halmashauri kupata mapato yatakayorudi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii inayorahisisha ukuaji wao kiuchumi kuzia kipato cha mtu mmoja, familia, kaya, mtaa, kijiji na taifa kwa ujumla.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu imara ya barabara, ujenzi wa vituo vya afya, miundombinu ya elimu na maji kwa ajili ya ustawi wa maisha yao na maendeleo.

